

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mkuu wa TAKUKURU (M) Simiyu

S.L.P 306, Simiyu

Simu: (028) 2700374 Nukushi (028) 2700532

Barua pepe:rbcsimiyu@pccb.go.tz

Wavuti www.pccb.go.tz

22/04/2020

MAAFISA WATATU KORTINI KWA UBADHIRIFU WA MILIONI 24

APRILI 20, 2020

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa – TAKUKURU Mkoa wa Simiyu, kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka mkoani humo, imewafikisha mahakamani, Watumishi watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega mkoani Simiyu.

Washitakiwa hao wamefikishwa Mahakamani wakishitakiwa kwa makosa mawili ya ubadhirifu wa shilingi 24,974,000/- za mradi wa upimaji wa viwanja wilayani Busega.

Washitakiwa hao, Magesa Aspenas Magesa (41) ambaye ni Afisa Ardhi, Raymond Jackson Mahendeka ambaye ni Fundi Mchundo na Augutina Morce Kitau (42) Mhasibu Msaidizi walisomewa mashtaka dhidi yao katika Mahakama ya Wilaya ya Bariadi na Wakili wa Serikali mnamo Aprili 20, 2020 ambapo walikana mashitaka hayo.

Katika shitaka la kwanza ilielezwa Mahakamani hapo kuwa kati ya Juni 04 na Septemba 30, 2019 katika eneo la Nyashimo wilayani Busega washitakiwa hao kwa pamoja waliandaa hati ya malipo ya uongo ikionesha kuwa viwanja 2,200 vilivyopo Kata za Mkula, Lamadi na Nyamikoma kuwa imesainiwa na watu mbalimbali na kufanikiwa kulipwa bila uhalali wowote kiasi cha shilingi 24,974,000/- jambo ambalo si kweli na kinyume na vifungu namba 333,335(d)(i) na 337 vya Kanuni ya Adhabu.

Aidha **katika shitaka la pili** ilielezwa kuwa washitakiwa kwa pamoja kati ya tarehe tajwa walifanya udanganyifu kwa kutumia hati ya malipo namba 473116V1902668 iliyokuwa na kiasi

cha shilingi 42,524,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 24,974,000/- zilikuwa ni malipo hewa. Kosa hili ni kinyume na vifungu namba 342 na 337 vya Kanuni ya Adhabu.

Pamoja na kukana mashitaka hayo, washitakiwa wa pili na wa tatu walishindwa kutimiza masharti ya dhamana ambayo yalimtaka kila mshitakiwa awe na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa Serikali ambao watasaini dhamana ya shilingi milioni 10 kila mmoja na kuwasilisha hati zao za kusafiri. Mshitakiwa wa tatu alitimiza masharti hayo. Kesi hiyo namba 57 ya mwaka 2020 imeahirishwa hadi Mei 04, 2020 kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali.

Imetolewa na Mkuu wa Takukuru (M) Simiyu.